# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI

**08 MEI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA ISHIRINI – TAREHE 08 MEI, 2025

**I. DUA:**

**II. TAARIFA YA SPIKA:**

**III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## IV. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**252 MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ipi kauli ya Serikali juu ya upungufu mkubwa wa Watumishi wa Kada ya Afya na Walimu Wilayani Kalambo.

**253 MHESHIMIWA MWANTUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza kuwapatia Mikopo Wajasiriamali wadogo Wanawake na Vijana.

**254 MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanzisha ujenzi wa Barabara ya lami ya Mwanama - Kanisani kwenye Kata ya Olorien Jijini Arusha.

**WIZARA YA NISHATI:**

**255 MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itaongeza Jenereta katika Wilaya za Mpanda na Tanganyika ili kuondoa tatizo la kukatika umeme mara kwa mara.

**WIZARA YA KILIMO:**

**256 MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali kupitia Bodi ya Korosho ina mpango gani wa kuwapatia Wakulima Ruzuku ya Pembejeo Mikoa iliyoanza kulima zao la Korosho.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**257 MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Tarime itajengwa ili kuwezesha ufanisi wa utendaji kazi wa Idara hii muhimu.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**258 MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itakamilisha zoezi la urasimishaji wa maeneo ya *Squatters* katika Jimbo la Kinondoni.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**259 MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga Minara ya Mawasiliano Wilayani Kyela katika maeneo ya mpakani mwa Nchi ya Malawi.

**WIZARA YA AFYA:**

**260 MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali italipa madeni ya Mfuko wa Bima ya Afya NHIF inayodaiwa na watoa huduma baada ya tathimini kufanyika.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**261 MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya mgogoro wa mipaka baina ya Wananchi wa Kijiji cha Ngombo na TAWA – Malinyi.

**V. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA MAJI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **08 MEI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |